**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA

**16 MEI, 2025**

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA – TAREHE 16 MEI, 2025

### I. DUA:

### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa

Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**330 MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Namwanga baada ya Halmashauri ya Masasi kuanza ujenzi.

**331 MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Barabara za Isenyela - Sangambi - Lupa - Lualaje na Chunya Godima - Sangambi kuwa chini ya TANROADS.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**332 MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, upi mpango wa kuwapandisha Madaraja kwa Mserereko Walimu wenye changamoto ya kupandishwa Madaraja wakiwemo wa Kakonko.

## WIZARA YA MAJI:

**333 MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Mto Rufiji utaanza baada ya upembuzi yakinifu kukamilika.

**334 MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni miradi gani ya maji inatekelezwa Kyerwa, Mkandarasi ni nani, inagharimu kiasi gani na lini itakamilika.

## WIZARA YA AFYA:

**335 MHESHIMIWA BERNADETA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha Sekta zote zinashiriki vita dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza yanayosababisha vifo vingi nchini.

**336 MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007 inayosema akina Mama Wajawazito watajifungua bure bila malipo bado ipo.

**337 MHESHIMIWA ALI JUMA MOHAMED (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kwa nini michango ya Bima ya Afya isiwe sawa na utaratibu wa michango ya Pensheni kati ya Mwajiri na Mtumishi.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**338 MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Majosho ya kuogeshea Mifugo kwenye Vijiji vya Jimbo la Singida Mashariki.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **16 MEI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |